



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

OFISI YA NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO
TAALUMA, UTAFITI NA USHAURI



WITO KWA AJILI YA MAOMBI YA UDAHILI NA UFADHILI WA MASOMO YA
SAYANSI KATIKA PROGRAMU MAALUMU YA MSINGI KWA
WANAFUNZI WA KIKE

A: UTANGULIZI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza mradi wa miaka mitano (2021/2022-2025/2026) wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (Higher Education for Economic Transformation (HEET)). Kupitia mradi wa HEET Wizara imetenga fedha kwa ajili ya ufadhili wa masomo katika Programu Maalumu ya Msingi kwa wanafunzi wa kike waliopungukiwa na sifa kidogo za kujiunga na masomo ya elimu ya juu katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STUH). Programu maalumu hiyo itatolewa katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (CKHT) kuanzia mwezi Agosti, 2023. Wanafunzi watakaohitimu na kufauli masomo katika programu hii maalumu kwa viwango vilivyowekwa watapata sifa za kuomba udahili katika taasisi za Elimu ya juu nchini kwa kufuata taratibu zilizoainishwa na TCU, NACTIVET na Chuo husika kwa mwaka wa masomo 2023/2024 ikiwa ni pamoja na sifa za kuomba mkopo wa masomo ya elimu ya juu kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania bara na Tanzania visiwani. Waombaji wanaotoka katika familia masikini zinazohudumiwa na TASAF, walemavu na yatima watapewa kipaumbele.

CKHT kinayo furaha kutangaza nafasi za ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa kike wenye sifa zinazohitajika ili kujiunga na programu hii maalumu.

B: SIFA ZA KUJIUNGA

Muombaji ataweza kukubaliwa kujiunga kwenye programu husika endapo atakuwa na sifa au vigezo vingine muhimu vifuatavyo:

- Cheti cha Mtihani wa Elimu ya Sekondari (**Kidato cha NNE**) kikiwa na ufaulu angalau kwenye masomo manne ambayo yamepatikana kabla ya kufanya mtihani wa juu wa elimu ya sekondari au ufaulu unaofanania na chochote kati ya vifuatavyo:
- Cheti cha Juu cha Mtihani wa Elimu ya Sekondari (**Kidato cha SITA**) kwenye tahasusi mojawapo kati ya PCB, PCM, CBG, PGM, PMC na EGM na kuwa na ufaulu wa angalau pointi 1.5 kutoka kwenye masomo mawili ya sayansi katika tahasusi tajwa
AU
- Stashahada katika programu ya **STUH** kutoka kwenye chuo kinachotambulika yenye ufaulu wa GPA ya 2.0 mpaka 2.9.
AU
- NTA Level 5/Professional Technician Level II Certificate.

C: NJIA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI

Programu hii itafundishwa kwa njia ya ana kwa ana pamoja na matumizi ya mtandao kupitia miundombinu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

D: MAENEO YA UFADHILI

Ufadhili utazingatia maeneo yafuatavyo: ada ya masomo, gharama za chakula na malazi, vifaa vya kujifunzia, shajara, bima ya afya, kishikwambi, vifaa visaidizi kwa wanafunzi wenye ulemavu na nauli ya kutoka nyumbani na kwenda kituo cha mafunzo na kurudi nyumbani baada ya kuhitimu.

E: UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

Muombaji anapaswa kujaza fomu ya maombi ambayo inapatikana kwenye vituo vyote vya mikoa vya CKHT bara na visiwani (Unguja na Pemba). Fomu ya maombi inapatikana pia kwenye tovuti ya CKHT. Fomu ikishajazwa irudishwe kwenye kituo cha mkoa husika. Mwombaji pia anaweza kutuma fomu yake ya maombi baada ya kuijaza kupitia barua pepe ya ofpheet@out.ac.tz. Hakuna ada ya udahili.

F: MWISHO WA MAOMBI

Mwisho wa maombi ni tarehe **Agosti 5, 2023**

Imetolewa na Ofisi ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo
Taaluma, Utafiti na Ushauri